Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA

LA MTANDAONI | TOLEO LA FEBRUARI 2023

## NSSF YAANDIKA HISTORIA NYINGINE YA MAFANIKIO




Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

Simu Bure
0800116773

@NssfTanzania




# NSSF yaandika historia nyingine ya mafanikio

## *Mkurugenzi Mkuu asema Mfuko upo imara na endelevu

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umeandika historia nyingine mpya na kubwa ya mafanikio ambapo ndani ya kipindi cha miaka miwili ya uongozi makini wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, thamani ya Mfuko imeongezeka na kufikia shilingi trilioni 6.6 mwezi Desemba 2022, ikiwa ni ongezeko la asilimia 36 kutoka shilingi trilioni 4.7 iliyokuwa mwezi Machi, 2021.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, amesema hayo tarehe 8 Februari, 2023 mbele ya waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Mfuko katika ukumbi wa Idara ya Habari (MAELEZO), uliopo katika jengo la PSSSF Makole jijini Dodoma.

“Ongezeko hili linatokana na kuongeza michango ya wanachama pamoja na mapato yatokanayo na uwekezaji, hivyo ukuaji huu wa Mfuko unathibitisha kuwa NSSF ipo imara na endelevu kwa ajili ya utoaji huduma za hifadhi ya jamii nchini,” amesema Mshomba.

Amesema katika mwaka wa fedha unaoishia mwezi Juni 2023, Mfuko unatarajia kukusanya michango ya shilingi trilioni 1.6 ambayo ni ongezeko la asilimia 14 ukilinganisha na michango ya shilingi trilioni 1.4 kwa mwaka 2021/22.

# *Mkurugenzi Mkuu ampongeza Dkt. Samia kwa kuwa chachu ya ongezeko la Wawekezaji

**Na MWANDISHI WETU**

Mshomba amesema mapato yatokanayo na uwekezaji kwa mwaka 2022/23 yanatarajiwa kuendelea kuwa shilingi bilioni 700 kiasi ambacho ni ongezeko kubwa ukilinganisha na miaka ya hivi karibuni ambapo mapato hayo yalikuwa chini ya shilingi bilioni 500.

Amesema faida kwa mwaka 2022/23 inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 1.27 ukilinganisha na faida ya shilingi trilioni 1.01 kwa mwaka 2021/22.

Mshomba amesema katika mwaka wa fedha unaoishia mwezi Juni 2023, Mfuko unatarajia kufikisha wanachama wachangiaji 1,249,865 ikiwa ni ongezeko la asilimia 20 ukilinganisha na wanachama wachangiaji 1,039,183 waliokuwepo katika Mfuko mwezi Juni 2022.

Amesema katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 2023, thamani ya vitega uchumi vya Mfuko inatarajiwa kukua na kufikia shilingi trilioni 6.3 ambayo ni ongezeko la asilimia 17 ukilinganisha na thamani ya shilingi trilioni 5.4 iliyokuwa mwezi Juni 2022.

Aidha, amesema katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 2023, Mfuko unatarajia kulipa mafao ya shilingi bilioni 769.3 ambayo ni ongezeko la asilimia 17 ukilinganisha na shilingi bilioni 659.8 zilizolipwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022.



Muonekano wa sehemu ya Kiwanda cha Sukari Mkulazi kilichopo Mkoani Morogoro ambacho ni kampuni Hodhi inayomilikiwa kwa ubia baina ya NSSF na Kampuni ya uzalishaji mali ya Jeshi la Magereza




**Inaendelea ..............**

"Katika eneo hili la mafao napenda kumshukuru tena Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia ombi la vyama vya wafanyakazi kupitia TUCTA la kuja na kikokotoo kipya kwa ajili ya manufaa ya wastaafu wetu ambacho kilianza kutumika mwezi Julai, 2022," amesema Mshomba.



Amesema juhudi mbalimbali za kuvutia wawekezaji na kufungua fursa mpya za biashara umeuwezesha Mfuko kuongeza wastani wa makusanyo ya mwezi na kufikia shilingi bilioni 118 kwa mwezi katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022, sawa na asilimia 14.

Taarifa hiyo kwa vyombo vya habari ni muendelezo wa mikutano inayoandaliwa na Idara ya Habari (MAELEZO) kwa ajili taasisi za Umma kueleza mafanikio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/23.

# TAARIFA KWA UMMA

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

## ZOEZI LA UHAKIKI WA WASTAAFU NA WATEGEMEZI

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unawatangazia wastaafu na wategemezi wote wanaolipwa pensheni ya kila mwezi kuwa, kutakuwa na zoezi la uhakiki lililoanza tarehe **1 Februari 2023** hadi **28 Aprili 2023,** Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa **2:30 asubuhi** hadi saa **10:30 jioni** kwenye ofisi zetu za NSSF za mikoa yote. Kwa wastaafu waliopo Unguja na Pemba uhakiki wao utafanyika ofisi ya ZSSF. Aidha wastaafu waliopo Dar es Salaam uhakiki utafanyika katika ofisi zetu za Mkoa ambazo ni Ilala, Temeke, Kinondoni (Ubungo), Mbezi Beach na Kigamboni.

**Mstaafu anatakiwa kufika na nyaraka zifuatazo:**

1) Kitambulisho cha NSSF au kuponi
2) Kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA
3) Picha moja ndogo ya sasa ya rangi (passport size) kwa wale ambao hawakufanya uhakiki mwaka 2022
4) Kwa wategemezi (watoto) tafadhali fika na cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha shule.

Aidha, malipo ya pensheni ya kuanzia **mwezi Juni 2023** yatafanyika kwa wastaafu ambao wamehakikiwa tu. Kwa wastaafu wagonjwa au wazee wasiojiweza taarifa itolewe kupitia barua pepe **customercare@nssf.go.tz** au piga simu ya bure **0800116773.**

**Kwa mawasiliano zaidi fika ofisi ya NSSF iliyo karibu nawe.**

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma**

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF